JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AWAMU YA TATU YA KAMPENI YA CHANJO YA POLIO YA MATONE DHIDI YA UGONJWA WA POLIO NCHINI

**Dodoma, 30 Agosti, 2022.**

**Ndugu wanahabari;** Wizara ya Afya imekuwa ikitoa taarifa kwa wananchi mara kwa mara kuhusiana na mwenendo wa magonjwa mbalimbali ya milipuko nchini na hatua zinazochukuliwa kukinga na kudhibiti magonjwa hayo ikiwemo ugonjwa wa Polio.

**Ndugu wanahabari;** Ugonjwa wa Polio ni ugonjwa unaosababishwa na kirusi ambacho huambukizwa kutoka kwa mtu aliyeathirika kwenda kwa mwingine kwa kula au kunywa kitu kilichochafuliwa na kinyesi chenye virusi vya Polio.

Virusi vya Polio vinapoingia mwilini huathiri mfumo wa fahamu na kusababisha madhara kiafya ikiwa ni pamoja na kupooza kwa ghafla kwa kiungo au viungo na hata kupelekea kifo. Dalili za awali za Ugonjwa wa Polio ni pamoja na homa, uchovu, maumivu ya kichwa, kutapika, kukakamaa shingo na maumivu ya viungo. Ugonjwa wa Polio hauna tiba. Njia kuu ya kuzuia ugonjwa huu ni kuwapatia chanjo ya Polio watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano. Chanjo hizi zimekuwa zikitolewa kupitia vituo vya kutolea huduma za afya na kwa njia ya mkoba na kliniki tembezi.

**Ndugu wanahabari;** Mnamo tarehe 17 Februari 2022 Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitoa taarifa ya uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa Polio (*Wild polio Virus*) nchini Malawi. Hadi sasa Malawi imeripoti visa viwili (2) toka mlipuko huu utangazwe Mwezi Februari, 2022. Aidha, nchi ya Msumbiji imeripoti visa vinne (4) ambapo kisa cha kwanza nchini humo kiliripotiwa mnamo Mwezi Mei, 2022.

**Ndugu wanahabari;** Kufuatia kuonekana kwa ugonjwa huu wa Polio katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitoa tamko kuwa Ugonjwa wa Polio ni janga la Kimataifa (*Public Health Emergence of International Concern*). Hii ikiwa na maana kuwa kugundulika kwa mtoto mmoja mwenye ugonjwa huu kuna uwezekano wa uwepo wa watoto zaidi ya mia mbili wenye maambukizi na uwezo wa kuambukiza watoto wengine na hata watu wazima ambao hawajapata chanjo.

**Ndugu wanahabari; Shirika la Afya Duniani (WHO) linaelekeza kuwa unapotokea mlipuko au tishio la mlipuko wa ugonjwa wa Polio nchini, nchi husika na nchi jirani zinapaswa kufanya Kampeni ya kutoa chanjo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) kwa awamu nne mfululizo** ili kila mtoto aweze kupata kinga kamili. Utaratibu wa kuhakikisha watoto wote wanapata kinga kamili hufanyika kupitia kampeni ya utoaji chanjo kwa watoto kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, kupitia nyumba kwa nyumba, na kuwafuata watoto popote walipo kwa mfano katika magulio au minada, shule za awali, vituo vya usafiri, nyumba za ibada sehemu za wazi za michezo na sehemu yoyote ambapo mtoto anaweza kupatikana.

**Ndugu wanahabari;** Kufuatia mlipuko wa ugonjwa huu katika nchi za Malawi na Msumbiji, na kwa kuzingatia ukaribu wa kijiografia na

mwingiliano wa watu kati ya Tanzania, Malawi na Msumbiji kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, kuna uwezekano mkubwa wa maambukizi ya Ugonjwa wa Polio kusambaa na kuingia nchini kwetu. Hivyo ili kuweza kudhibiti ugonjwa huu usiingie nchini na kwa kuzingatia Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wadau wa huduma za chanjo nchini inatekeleza Kampeni ya kutoa Chanjo ya Polio kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**Ndugu wanahabari;** ***Awamu ya kwanza ya Kampeni*** ilifanyika kuanzia tarehe 24 hadi 27 Machi 2022 na ilitekelezwa katika mikoa minne inayopakana na nchi ya Malawi ambayo ni Mbeya, Songwe, Njombe na Ruvuma. Kampeni hii ililenga kuwafikia watoto **975,839** wenye umri chini ya miaka mitano, na kufanikiwa kuwafikia watoto **1,130,261** sawa na asilimia **115** ya walengwa wote. ***Awamu ya pili ya Kampeni*** hii ilifanyika nchi nzima kuanzia tarehe 18 hadi 21 Mei, 2022 ikilenga kuwafikia Watoto **10,295,316** wenye umri chini ya miaka mitano, na kufanikiwa kuwafikia watoto **12,131,049** sawa na asilimia **117.8** ya walengwa wote.

**Ndugu wanahabari;** Wizara inawapongeza na kuwashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Wataalamu wa Afya, Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa, Vyombo vya Habari na wananchi kwa kufanikisha vyema utekelezaji wa Kampeni hii kwa awamu ya kwanza nay a pili.

**Ndugu wanahabari;** Sasa tunaelekea kufanya ***Awamu ya tatu ya Kampeni ya kutoa chanjo ya matone ya Polio*** ambayo itaanza terehe 1 hadi 4 Septemba, 2022 na zoezi hili litakuwa nchi nzima.

Awamu hii ya tatu tumelenga kuwafikia Watoto **12,386,854** wenye umri chini ya miaka mitano.

**Ndugu wanahabari;** Chanjo ya Polio ya matone inayotolewa wakati wa Kampeni, ni chanjo inayotolewa siku zote katika ratiba ya kawaida ya chanjo za watoto katika vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Ninatoa wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini kupitia Kamati za Afya msingi za Mikoa na Halmashauri kusimamia kampeni hii ili kumfikia kila mtoto popote alipo kwa lengo la kuhakikisha kila mtoto anapata kinga na kuzuia Ugonjwa huu usiingie nchini kwetu. Aidha, ninatoa wito kwa Wazazi/Walezi, Taasisi za Umma, Binafsi, Dini, Asasi za Kiraia, Wawakilishi wa makundi mbalimbali ya Kijamii, Vyombo vya Habari na wananchi kwa ujumla kushirikiana na Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika utekelezaji wa kampeni hii.

Niwasihi na kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa timu za wachanjaji watakapofika katika maeneo yenu, kupita nyumba kwa nyumba na maeneo yote alipo mtoto wa chini ya miaka mitano.

Imetolewa na:



Ummy A. Mwalimu (MB)

**WAZIRI WA AFYA**